

Ufundishaji wa Fasihi-Tafsiriwa kwa Kiswahili katika Vyuo Vikuu nchini Kenya

Joseph Nyehita Maitaria
Chuo Kikuu cha Karatina

Ikisiri

Fasihi-tafsiriwa zinafunzwa katika idara za Kiswahili za vyuo vikuu nchini Kenya. Aidha, zimekuwa zikifuzwa kama mojawapo ya kozi za lazima au ya hiari. Baadhi ya wanafunzi huliendeleza somo hili kwa kufanyia utafiti katika shahada ya uzamili na uzamifu. Kozi hii hufundishwa kama kozi inayojisimamia au baadhi ya vitabu teule hujumuishwa katika kozi za fasihi ya Kiswahili. Swali ni, malengo ya kufundisha kozi hizi ni yepi katika idara za Kiswahili za vyuo vikuu? Aghalabu mafunzo hayo hugusia zaidi maudhui yanayowasilishwa na kunga zalizotumiwa katika uwasilishaji. Azma ya makala hii ni kutathmini namna fasihi-tafsiriwa ya kigeni inavyofuzwa katika Idara za Kiswahili katika vyuo vikuu nchini Kenya. Kadhalika, imependekezwa namna ufunzaji huo unavyoweza kuelekezwa zaidi katika kukabiliana na upungufu uliopo.

Maneno Muhimu: Ufundishaji, Fasihi-Tafsiriwa, Kiswahili

Utangulizi

Kwa mujibu wa Ruhumbika (1983), tafsiri za fasihi za lugha nyingine ni hazina kubwa hasa katika mataifa yanayoendelea. Kadhalika, anaeleza kuwa maandishi ya kigeni hutafsiriwa kwa sababu ya umuhimu wa yale yaliyomo. Hata hivyo, mawazo hayo yalikuwa yanashikilia nafasi muhimu katika miaka ya 1980. Katika miaka hiyo, fasihi ya Kiswahili ilikuwa katika hatua ya kujilea na kujikuza. Ryanga (1985) anaeleza kuwa, katika miaka ya 1980 katika Idara ya Isimu na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Nairobi, kulizuka mjadala kuhusu vitabu vilivyotafsiriwa na kukubaliwa kwavyo katika fasihi ya Kiswahili. Kwa kurejelea mjadala huo, hoja mbili zilitolewa: kwamba, vitabu vilivyotafsiriwa havina nafasi katika fasihi ya Kiswahili na kwamba, tafsiri hizo zinaiua fasihi ya Kiswahili badala ya kuiendeleza. Sababu zilizotolewa ni kwamba: fasihi asilia zilizoandikwa kwa lugha nyingine na kutafsiriwa kwa Kiswahili ilikosa mnato wa kisani; kazi hizo hutumia lugha ya kiwango cha chini na lugha ikilinganishwa na lugha katika tungo asilia.

Katika ufunzaji wa fasihi-tafsiriwa za kigeni kwa Kiswahili kwenye idara za vyuo vikuu, mwanafunzi huwekwa kwenye nafasi ya nne (kuna watunzi asilia, waliotafsiri, wahadhiri wanaofunza na wanafunzi ambao ni walengwa). Swali hapa

ni: ujumbe unawasilishwa vyema au unapotoshwa kaupitia kwa fasihi-tafsiriwa za kigeni kwa Kiswahili? Hapa ieleweke kuwa, vitabu hivyo ni vile vilivyotafsiriwa na wala si asilia. Hivyo, ni vigumu kuwa na uhakika kuhusu ubora wa kazi hizo au ujuzi wa wahadhiri husika kuhusu kazi asilia. Namna na jinsi wahadhiri wanavyofunza huwa na athari kubwa kwa wanafunzi ambao ni wataalam na walimu watarajiwa katika siku za usoni. Baadhi ya maswali yanayoweza kuulizwa ni: kuna haja ya kuvifunza vitabu hivyo? Vitabu hivyo vinapaswa kufunzwa vipi kwa sasa? Makala hii inatathmini namna fasihi-tafsiriwa za kigeni kwa Kiswahili zinavyofunzwa katika vyuo vikuu nchini Kenya. Mwishowe, inapendekezwa namna ya kukabiliana na baadhi ya upungufu uliopo kwa sasa katika Idara za Kiswahili.

Uchanganuzi wa Data

Data iliyochanganuliwa imetokana na majibu ya hojaji kwa wanafunzi 30 kutoka vyuo vikuu sita nchini Kenya (watano kutoka kila chuo): vyuo vya umma vitatu na vitatu vya kibinafsi. Kadhalika, wakufunzi 6 walihojiwa: wawili wanaofunza kozi ya tafsiri; na wawili wanaofunza fasihi linganishi). Pia, wahakiki wa fasihi walihojiwa kupitia mawasiliano ya arafa za simu na barua pepe. Kutokana data iliyokusanywa na kuchanganuliwa, ilibainika kuwa kozi hizi zipo katika mitaala ya vyuo. Kwa ambavyo ni kozi za hiari; wanafunzi wachache mno huzichagua. Kwa maana hii, kozi hizo huweza kufunzwa ingawa wakati mwingine hazifunzwi. Vilevile, ilibainika kuwa baadhi ya vitabu vya fasihi-tafsiriwa kwa Kiswahili hufunzwa katika miktadha ya masomo mengine. Kwa mfano, kozi hizo hutumiwa kama matini za kuchanganuliwa katika kozi za tafsiri, kozi za fasihi linganishi na kozi teule za fasihi ya Kiswahili. Kutokana na hojaji zilizotokana na wanafunzi, matarajio yao ni kuwa wataalam wa tafsiri na ukalimani. Huo ndio msukumo wa kujisajili katika kozi ya fasihi-tafsiriwa za kigeni kwa Kiswahili. Baadhi ya wanafunzi walilalamika kuwa, wanasoma vitabu hivyo kwa kuzingatia maudhui na kwa ajili ya mtihani mwishoni mwa muhula. Aidha, wanafunzi walieleza kuwa hawajawahi kuviona vitabu asilia na kuwa wanategemea tafsiri ya kazi hizo.

Fasihi-Tafsiriwa kwa Kiswahili katika Muktaba wa Fasihi ya Kiswahili

Fasihi-tafsiriwa ni utanzu wa fasihi zinazotungwa kwa lugha asilia na kuwasilishwa kwa lugha lengwa. Hivyo, hujaribu kuhamisha ujumbe, maana na taathira zote za kifasihi kwa lugha pokezi. Kulingana na Mwansoko (1996) na Newmark (1988), tafsiri ni zoezi la uwasilishaji wa mawazo kutoka matini ya lugha asilia hadi kugha pokezi. Kifasihi, tafsiri hizo ni daraja linalounganisha hadhira au wasomaji wanaotumia lugha zinazotofautiana. Fasihi-tafsiriwa ya Kiswahili ina historia ndefu Afrika hapa Mashariki. Maendeleo hayo yanaweza kueleweka kwa kuzingatia vipindi vitatu: Majilio ya wageni wa awali (Waarabu na Wamisheni); wakati wa ukoloni na baada ya kutenguliwa kwa utawala wa ukoloni. Kirasmi, fasihi-tafsiriwa ilianza kushughulikiwa katika utawala wa ukoloni wa Waingereza mnamo 1925. Kabla ya wakati huo, Kiswahili tayari kilikuwa kimekita mizizi katika mawasiliano

ya wenyeji wa Afrika Mashariki (Shitemi, 1997; Mbaabu, 1996). Katika miaka hiyo, sera ya lugha ya utawala huo ilihitaji vitabu vilivyoandikwa kwa Kiswahili. Juhudi hizo za awali zilichangia kuwapa kwa vitabu vilivyohitajika ili kukidhi mahitaji ya kielimu (Maitaria na Momanyi, 2016). Wakati huo, vitabu vya fasihi ya Kiswahili vilivyotungwa na wenyeji vilikuwa vichache mno lakini kwa sasa kuna vitabu vingi. Fasihi-tafsiriwa kwa Kiswahili za awali zilikuwa za hadithi fupi zilitafsiriwa kutoka kwa lugha ya Kiarabu. Miongoni mwa kazi hizo ni *Alfu Lela Ulela* na *Visa vya Abumuwasi*. Zaidi ya kuburudisha, kazi hizo zinawasilisha maudhui ya kimaadili. Katika kipindi cha sasa, fasihi za kigeni zinaendelea kutafsiriwa na kutumiwa katika viwango mbalimbali vya vya elimu; kuanzia madarasa ya chini ya chekechea. Kwa sasa, kuna kazi anuwai za fasihi-tafsiriwa za ndani na nje ya bara la Afrika kutokana na juhudi za wataalamu wa lugha na fasihi. Matokeo ni kwamba, fasihi ya Kiswahili imepata sura mpya (Kandagor na Magugu, 2017). Swali ni, fasihi-tafsiriwa kwa Kiswahili zinafunzwa vipi katika vyuo vikuu? Katika kujibu swali hili, inafafanuliwa namna baadhi ya vitabu hivyo huteuliwa na mbinu zinazotumika katika ufundishaji. Fasihi-tafsiriwa za Kigeni kwa Kiswahili zilizopo kwa sasa zinaweza kuwekwa katika matapo mawili: zile zinazotokana na baadhi ya lugha za barani Afrika na zile za kutoka nje ya bara hili. Nyingi ya fasihi hizo za kigeni zilitokana na lugha asilia za kikoloni.

Dhima ya Kufundisha Fasihi-Tafsiriwa katika Vyuo Vikuu

Mojawapo ya malengo ya mitaala ya vyuo vikuu ni kuwatarisha wanafunzi kuwa wataalamu bora katika taaluma zao ili kuhudumia jamii na kuchangia katika maendeleo ya taifa (Kandagor na Magugu, 2017). Kuhusu dhima ya tafsiri, Ryanga na Ngowa (2013) wanaeleza kuwa, kazi mbalimbali za fasihi-tafsiriwa kwa Kiswahili zinachangia maendeleo na uhusiano mwema miongoni mwa wanajamii. Kwa misingi hiyo, mitaala katika vyuo vikuu inayotambua umuhimu huo zinapania kutekeleza malengo hayo. Mitaala hiyo ina kozi za Tafsiri, Fasihi-Tafsiriwa na Fasihi ya Kiswahili. Katika maeneo hayo matatu ndimo somo la fasihi-tafsiriwa kwa Kiswahili hujumuishwa. Kwa sasa, somo linalohusu vitabu hivyo vinafundishwa katika daraja ya shahada ya kwanza, uzamili na uzamifu. Swali hapa ni, dhima ya fasihi-tafsiriwa katika vyuo vikuu na hasa katika Idara za Kiswahili ni nini? Kimsingi, wanafunzi hao wanatarajiwa kuwa wataalam wa tafsiri au kupanua mtazamo na mawazo yao kuhusu fasihi ya Kiswahili? Kwa ujumla inaweza kuelezwa kuwa, malengo ni kuwafunza wanafunzi kuhusu yale yanayoendelea katika fasihi ambazo hazikutungwa kwa Kiswahili ila kwa kuzingatia mazingira ya Afrika Mashariki. Aidha, wanafunzi hao hawafahamu lugha asilia (au kigeni) iliyotumika katika uwasilishaji wa tungo hizo.

Baadhi ya wahakiki wa fasihi na lugha wana mwelekeo kwamba, fasihi - tafsiriwa kwa Kiswahili haina mchango wa kitaaluma katika fasihi ya Kiswahili na kiumbuji, kiwango cha chake ni cha chini. Maoni ya Muigai (2005) na Mutie (1997) ni kwamba, hakuna kazi ya tafsiri inayoweza kuwa kamilifu. Kwa maana hii, vitabu vya fasihi-tafsiriwa vinaposomwa au vinapofunzwa kwa mwafaka huweza

kuendeleza kwa kiasi fulani fasihi katika muktadha wa kimataifa; uthamini wa maisha ya watu katika tamaduni zingine; watunzi hujijengea fikra mpya na kuzifanyia majaribio katika tungo zao. Vilevile, hufunzwa kwa kuzingatia muktadha wa mazingira ya kigeni na huifanya hadhira kuthamini tamaduni za kigeni na kulinganisha hali ilivyo katika mataifa ya Afrika Mashariki. Fasihi-tafsiriwa kwa Kiswahili hukuzwa na hupigwa jeki kimsamiati, kintindo na kimaudhui kupitia kwa kunga za uwasilishaji hizo. Kimsingi, fasihi hizo zinabainisha maisha ya watu katika mazingira na tamaduni tofauti ulimwenguni (Bakize, 2013). Kwa kuwa hugusia maisha ya watu, fasihi hizo zinaweza kufanana au zisifanane katika muktadha wa wenyeji wa Afrika Mashariki. Kwa sababu hii, wanafunzi wa somo la fasihi-tafsiriwa kwa Kiswahili hujengewa mazingira mapana kuhusu namna wanavyoweza kukabiliana na hali inayosawiriwa iwapo hali hizo zipo au zinapojitokeza katika siku za usoni. Mathalani tamthilia ya *The Government Inspector* ‘Mkaguzi Mkuu wa Serikali (Nikolai Gogol) kinazungumzia uzembe wa wasiasa, maovu ya kijamii na ufisadi ulioshuhudiwa katika kitongoji cha Urusi. Kwa kuzingatia wahusika wanavyosawiriwa na ujumbe unaowasilishwa, wanafunzi wa fasihi hii wanaweza kupatanisha uhalisi huo na yale yanayoshuhudiwa katika taifa. Kutokana na uelekezi wanaoupata darasani, wanaweza kuchangia katika kuzikabili changamoto au kutoa tahadhari kwa viongozi waliopo. Mifano mingine ya fasihi hizo ni *Mfalme Edipode*, *Shamba la Wanyama*, *Antigoni*, *Julias Kaizari* miongoni mwa zngine.

Ingawa kumekuwa na mielekeo na mitazamo mbalimbali ya kuilekezea kidole cha lawana fasihi-tafsiriwa za kigeni, kwa kiwango Fulani, zimechangia si haba katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili. Dhima ya fasihi hizo zinaweza kufafanuliwa kwa kuzingatia yafuatayo:

- i. Kutokana na maendeleo ya teknolojia, ulimwengu umekuwa kijiji ambapo lugha na tamaduni mbalimbali huathiriana. Hivyo, fasihi-tafsiriwa ya kigeni imeisaidia fasihi ya Kiswahili kimtazamo kwa kuzingatia yale yanayoendelea ulimwenguni;
- ii. Wahakiki wa fasihi-tafsiriwa huangazia nguvu na udhaifu wa kazi hizo zilizotafsiriwa na hivyo kushughulikia masuala ya kitaaluma katika suala zima la tafsiri;
- iii. Inahakikisha kuwapo kwa vitabu teule vya kufundishia, vya ziada na marejeleo ya msingi ili kukidhi mahitaji fasihi katika ngazi zote za elimu, kuanzia shule za chekechea hadi vyuo vikuu;
- iv. Fasihi-tafsiriwa imesaidia kwa kiwango fulani kufafanulia dhana na mawazo muhimu kwa Kiswahili na hivyo kuipa hadhi ya kitaifa na kimataifa. Hii inamaanisha kwamba, lugha ya Kiswahili ina uwezo wa kuwasilisha dhana na mawazo muhimu. Katika usomaji wa fasihi hizo, wanafunzi huweza kuwa wahakiki wa fasihi katika kitengo cha fasihi linganishi. Kadhalika, wanafunzi wanajengewa mazingira ya kutaka

- kusoma tungo asilia na matokeo ni kuwa watafiti na wataalamu katika taaluma ya tafsiri;
- v. Vitabu vya fasihi-tafsiriwa ni kichocheo na ukuzaji wa ubunifu miongoni mwa waandishi ‘wakongwe’ na wale chipukizi hasa kupitia kwa kunga na mizungu iliyotumiwa katika uwasilishwa;
 - vi. Kusambaza na kupashana habari ambapo ulimwengu wa leo ni kama kijiji kutokana na utandawazi ambapo jamii huathiriana na huingiliana kifikra, kitamaduni, kisayansi na kiteknolojia. Hivyo, fasihi hii ni ufunguo wa ushirikiano mwema;
 - vii. Ni njia mojawapo ya kubainisha na kuelimisha kuhusu mambo mbalimbali kama vile ufasidi katika jamii na namna ya kukabiliana na sura hizo zinapojitokeza. Miongoni mwa kazi hizo ni tafsiri ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (inashughulikia ufasidi na kutowajibika kwa viongozi katika nchi), *Mabepari wa Venisi* (ubarakala unavyojishaua katika jamii za watu kutokana na sera zinazuia usawa katika ugavi wa rasilimali na ulaghai unaotumiwa na wale wanaojiweza) na *Shamba la Wanyama* (uongozi wa kidhalimu unaolemaza mwafaka wa utawala wa kidemokrasia ambapo wenye uwezo hujichukulia kuwa vigogo na ‘miungu wadogo’ katika jamii) miongoni mwa masuala mengine; na
 - viii. Baadhi ya fasihi hizo zinaakisi masuala yenye mshabaha na yale yanayoshuhudiwa pia katika jamii za Afrka ya Mashariki. Hivyo, baadhi ya vipengele vinawasilishwa katika fasihi hizo vinaweza kupatikana katika muktadha wa wenyeji. Kwa mfano, suala la uzingativu wa utubora hufafanuliwa katika jamii mbalimbali (nguvu za wema dhidi ya ubaya na kwamba, malipo ya uovu ni papa hapa duniani) ni baadhi ya mambo ambayo bado yapo katika ulimwengu wa sasa. Mfano hapa ni kama vile, masuala ibuka, migongano ya kitabaka; mila na desturi ambazo zimepitwa na wakati (mathalani ukeketwaji wa wasichana); UKIMWI, ufasidi, ndoa, ukarimu, ujirani mwema, dhuluma dhidi ya umma wa kike na amani katika jamii na changamoto zake. Hivyo, hadhira ya fasihi-tafsiriwa huweza kupata mchango wa kujitathmini na kujihakiki.

Kimsingi, fasihi-tafsiriwa zinaweza kuwa na mitazamo ya kitaifa, kikanda na upana wa kimataifa. Kwa hivyo, zinaweza kusaidia katika kuuelewa ulimwengu katika muktadha finyu na pia katika upana wake (Pike, 1967). Mambo hayo ni yale yanayopatikana katika jamii mbalimbali ulimwenguni.

Fasihi-Tafsiriwa na Ufundishwaji wake katika Vyuo Vikuu Nchini Kenya

Fasihi-tafsiriwa kwa Kiswahili inafunzwa kwa namna mbili: kama kozi inayojisimamia au kupitia kwa kozi nyingine ya idara za Kiswahili katika vyuo vikuu nchini Kenya. Miongoni mwa vyuo hivyo ni: Catholic, Chuka, Egerton, Embu, Greaster, Jaramogi, Karatina, Kenyatta, Kibabii, Kirinyaga, Laikipia, Machakos, Maseno, Masinde Muliro, Moi, Mount Kenya, Nairobi, Rongo, South

Eastern, miongoni mwa vyuo vingine. Katika Chuo Kikuu cha Kenyatta kuna kozi kama vile AKS 203: Kitangulizi cha Nadharia na Zoezi la tafsiri 'Introduction to Theory and Practice of Translation', KIS 302: Nadharia za Uhakiki wa Fasihi 'Theories of Literary Criticism' na KIS 303: Riwaya na Tamthilia ya Kisasa ya Kiswahili 'Contemporary Kiswahili Novel and Play'. Katika idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi kuna kozi kama vile: CLK 102: Introduction to translation and interpretation, CLK 304: Zoezi la Tafsiri na Ukalimani 'Practical Translation and Interpretation', CLK 410: Tafsiri ya Fasihi 'Literary Translation', CLK 202: Modern Kiswahili Poetry and Drama, CLK 302: Literary Theories and Criticism of Kiswahili Literature, CLS 503: Theories of Literature and Stylistics; CLS 509: Advanced Translation (Elective). Katika idara ya Lugha, Chuo Kikuu cha Karatina kuna kozi kama vile: KIS 321: Comparative Kiswahili Literature, KIS 414: Modern Kiswahili Drama. Katika Chuo Kikuu cha Jaramogi Oginga Odinga kuna kozi kama vile AKI 305: Kiswahili Novel na AKI 403: Kiswahili Play. Katika chuo Kikuu cha Masinde Muliro kuna kozi kama vile: LEK 821: Kiswahili Drama; KIS 416: Kiswahili Prose; KIS 415: Comparative Literature in Kiswahili; KIS 400: Lugha na fasihi; KIS 315: Kiswahili Literary Studies na KIS 313: Theatre Arts in Kiswahili. Katika Chuo Kikuu cha Mount Kenya kuna kozi kama vile: MLA 5108: Theories of Literary Criticism and Textual Analysis; MLA 5206: Literary History and Literature in Kiswahili na MLA 6111 Contemporary Kiswahili Literature.

Katika kozi zilizotajwa hapo juu, ni chache mno ambazo zinafundisha Fasihi-tafsiriwa za kigeni kwa Kiswahili. Baadhi ya kozi hizo huwa na miongozo ya kufundishia ambapo kuna vitabu vya fasihi-tafsiriwa kwa Kiswahili na hufunzwa kana kwamba ni fasihi ya Kiswahili. Katika fasihi-tafsiriwa, kuna kazi mbalimbali kama vile Ushairi, tamthilia, riwaya na hadithi fupi. Miongoni mwa kazi zinazofunzwa mno katika vyuo vikuu nchini Kenya ni 'Mabepari wa Venisi', Julius Caesar 'Julius Kaizari', *Antigone* 'Antigoni' (William Shakespeare), na *Animal Farm* 'Shamba la Wanyama' (George Orwell). Hiyo ni mifano ya fasihi tafsiriwa kutoka nje ya bara la Afrika. Shabaha hapa ni kuweza kusomwa na hadhira pana katika jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Miongoni mwa kazi hizo ni kama vile: *The Government Inspector* 'Mkaguzi Mkuu wa Serikali' (Nikolai Gogol), *Merchant of Venice* 'Mabepari wa Venisi (William Shakespeare). Aidha kuna baadhi ya kazi maarufu za asili ya lugha za Kiyunani, Kifaransa au lugha nyinginezo ambazo zimeweza kutafsiriwa kwa lugha pokezi ya Kiingereza. Kazi hizo ni kama vile *Oedipus Rex* 'Mfalme Edipode' (Sophocles) kilichotafsiriwa na Samwel Mushi. Wanafunzi hufanya kozi hii kwa matarajio ya kuwa wataalamu katika kitengo cha tafsiri na kuwa watunzi ambao ni wabunifu wenye mtazamo mpana.

Kutokana na ufafanuzi uliotolea hapo juu, tunajiuliza: Fasihi-tafsiriwa ni tungo za fasihi tu au fasihi kwa ujumla? Katika ufundishaji wa tungo mbalimbali za fasihi-tafsiriwa, wahadhiri huzingatia zaidi mawazo, ujumbe au maudhui (yaliyomo) na yanayopewa nafasi ndogo ni umuundo na umaumbo wa kazi hizo. Pia, utanzu wa ushairi-tafsiriwa ni nadra kushughulikiwa katika kiwango cha shahada ya kwanza.

Isitoshe, nadharia za uhakiki zinazotumiwa katika kuchanganulia fasihi-tafsiriwa za kigeni huwa tata, na kwamba haziakisi mazingira ya Afrika.

Ufunzaji wa Fasihi-tafsiriwa kwa Kiswahili

Kulingana na Brown (2000), taaluma ya ufundishaji inahitaji maaandalizi yanayohusu stadi za kihatua. Kwa hivyo, maafikiyo ya mhadhiri katika ufundishaji wa fasihi-tafsiriwa huegemea mno kwenye misingi ya ufundishaji alivyojengewa awali, jitihada za kibinafsi na kujiendeleza kiwakati katika taaluma ya ualimu (McAthur, 1993). Huu ndio mchukulio wa kijumla katika ufunzaji wa fasihi-tafsiriwa za kigeni kwa Kiswahili. Kwa maana hii, mkufunzi anahitaji kuupa uhai ufunzaji wake kadiri hadi mwisho wa muhula. Matayarisho ya mwalimu hayajikiti katika kufahamu historia na miktadha ya kitamaduni iliyozaa tanzu asilia bali pia kuzingatia kunga zilizotumiwa katika uwasilishaji wa tungo hizo za kisanaa. Kwa mintoarafu hii baadhi ya maapendekezo ambayo yanaweza kuzingatiwa katika ufunzaji wa fasihi-tafsiriwa za kigeni kwa Kiswahili ni:

- i. Zifunzwe kama chombo cha kuchochea usomaji wa kiuhakiki na utafiti. Hivyo, wanafunzi wasiwe ni wasikilizaji tu bali wajumuishwe katika mazoezi zaidi ya kiutafiti;
- ii. Zifunzwe kwa kuwafanya wanafunzi kufurahia na kuburudika badala ya kuwa adhabu kwao;
- iii. Muktdha wa tungo asilia ueleweke kabla na mkufunzi hajaanza kufundisha. sababu ni kwamba, wanafunzi humtegemea zaidi mhadhiri wao. Haipaswi kushikilia na kukubali yale yote yanayowasilishwa katika fasihi hizo bila kuhoji;
- iv. Wahadhiri wasiwe ni vipaza sauti kupitia fikra ngeni kwa kutumia Kiswahili kama chombo cha mawasiliano;
- v. Vitabu vinavyoteuliwa viwe vile vilivyoidhimishwa katika idara na wala visiwe ni vile anavyopendekeza mhadhiri binafsi;
- vi. Yaliyomo katika kazi hizo ni muhimu kuzingatiwa lakini pia kuna haja ya wanafunzi kuelekezwa kuhusu dhima ya fasihi-tafsiriwa, historia na utamaduni asilia; na
- vii. Kuna haja ya kujiuliza iwapo vinachangia katika fasihi ya Kiswahili.

Jukumu la Fasihi ni nini?

Fasihi ni sanaa inayobuniwa kutoakana na mazingira halisi ya maisha katika muktdha wa utamaduni wa jamii. Kimsingi, kuna ukuruba mkubwa kati ya lugha na maudhui yanayowasilishwa. Pamoja na mtindo unatumia na msanii huathiri kwa kiwango kikubwa upokezi wa ujumbe wa tungo za fasihi. Ingawa fasihi inaweza kuchukuliwa kuwa, kioo kinachobainisha maono ya watu katika muktdha wa utamaduni wa wenyeji, inaweza kutekeleza mambo mawili katika jamii: kuelimisha kutokana na yale yasiyojulikana au yanayojulikana ingawa

yamepuuzwa. Kadhalika, huweza kuwasilisha ujumbe kwa kuzingatia itikadi ya mtunzi na matokeo ni upotoshaji wa hadhira na umma katika muktadha usioeleweka katika utamduni wa jamii. Zaidi ya kubainisha hali halisi kwa ubunifu, mtunzi wa fasihi hupendekeza au kubashiri ambapo huweza kuwa ya kuwezekana au yasiyowezekeka katika uhalisi wake. Kwa kufafanua zaidi wazo hilo Adungo (2018) ameeleza kuwa, fasihi haisawiri maisha halisi bali ni tokeo la ubunifu. Mtunzi ana uwezo wa kubuni visa na wahusika wake kwa njia ambayo haikanganyi hali halisi ya maisha. Kwa maana hii, malighafi inatumika kuwasilishia kazi za fasihi inatokana na jamii mahsusi.

Kulingana na mawazo ya Njogu na Wafula (2007), tapo hilo la kwanza ndilo linalosherekewa zaidi katika jamii na tapo la pili huelekezewa kidole cha lawama. Japo, fasihi huweza kutafsiriwa kwa lugha pokezi (kama vile Kiswahili) ni kielelezo na kiashiria cha uhalisi wa maisha, hisi na utamaduni na mazingira yakini yaliyomzunguka mtunzi asilia. Kulingana na Kamau (2018), fasihi haiigi kikasuku bali huiga kiubunifu kwa kuzingatia mambo yanayoathiri maisha ya binadamu. Kwa hivyo, mtafsiri wa kazi za fasihi ana wajibu wa kuwasilisha yale yanayopatikana katika kazi asilia bila ya kuingiza zaidi hisia zake. Mtafsiri anaweza kutoa maelekezo ili kuondoa viwingu vya utata. Baadhi ya watafsiri huzingatia zaidi uhuru alionao katika kufafanua baadhi ya vipengele vya lugha na ujumbe unaowasilishwa katika kazi asilia. Hii ni athari ambayo hubebeshwa fasihi-tafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Kadhalika, fasihi ni chombo cha kufafanulia utamaduni wa jamii; japo fasihi ni kazi ya kubuniwa, ni chombo cha kufunza, kutahadharisha na kuelekezea tamaduni, kusanisha. Isitoshe fasihi ni kioo cha maisha ya jamii kwa mtazamo wa tajriba ya wenyeji. Hata hivyo swali ambayo yanaweza kuulizwa ni: vitabu vya fasihi vinavyofundishwa vina umuhimu gani katika jamii ya sasa.

Maandalizi ya Awali kwa Mkufunzi wa Fasihi-Tafsiriwa

Baadhi ya wahadhiri wanaofunza masomo ya fasihi-tafsiriwa huwa ni walimu wa muda ambao hawajahitimu masomo yao ya uzamifu. Walimu hao wanapatikana sana katika mabewa (Mohochi, 2018). Tanzu za fasihi kama zilivyo sanaa zozote zile ni kazi zilizobuniwa na zilizojikita katika lugha teule. Kwa maana hii, tungo hizo huwasilishwa kwa tamathali za usemi zinazohitaji kufafanuliwa bila ya utata wa maana na ujumbe. Vilevile, kazi hizo zinaandamana na hisi au mchomo na utamaduni wa mwandishi asilia (Ruhumbika, 1985). Baadhi ya mifano ni: tamthilia ya *Animal Farm* ‘Shamba la Wanyama’ ya George Orwell (Tafsiri ya Fortunatus Kawegere) – imetumia mafumbo na kunga za fasihi simulizi ya kihurafa. Kazi nyingine ni *Merchant of Venice* ‘Mabepari wa Venisi’ ya William Shakespeare (Tafsiri ya Julius Kambarage Nyerere) – zaidi ya mafumbo na ni kazi ya kimajazi. Kulingana na Malangwa (2005) ni kwamba, tafsiri hii imezingatia mkabala wa itikadi-tawala ya ujamaa iliyozingatwa katika nchi ya Tanzania ambapo wafanyabiashara walifasiriwa kama mabepari na makabaila. Aidha, *The Government Inspector* ‘Mkaguzi wa Serikali’ ya Nikolai Gogol (Tafsiri ya Joshua

Samwel Madumulla) – imezingatia zaidi kinaya na kejeli. Ingawa kazi hizo ni fasihi-tafsiriwa na wahakiki wa fasihi, swali ni tafsiri hizo zilingatia itikadi au falsafa gani: ile ya mwandishi asilia au ya mtafsiri? Baadhi ya mambo hayo yanaweza kuathiri ufunzaji na upokezi wa wanafunzi wa Kiswahili katika vyuo vikuu. Maandalizi mwafaka ya mkufunzi yanahitaji kuzingatia mambo yafuatayo:

- i. Kutenga muda wa kuvipitia vitabu kabla hajaviteua ili kuhakikisha kuwa taratibu za tafsiri zimezingatiwa katika kazi hizo;
- ii. Kuhakikisha kuwa vitabu hivyo vimezingatia visawe vya miundo ya lugha asilia iliyotumiwa katika lugha pokezi. Kwa kufanya hivyo, mwanafunzi hatapata taabu katika kuelewa mawazo na ujumbe unaowasilishwa;
- iii. Ahakikisha kuwa malengo ya somo yamebainisha siyo tu katika faili yake bali pia kwa mwanafunzi;
- iv. Kazi hizo zinadhihirisha utamaduni asilia kwa kuuweka katika muktadha faafu katika ujumbe unaowasilishwa katika lugha pokezi kwa kuzingatia tajiriba na uhalisi wa maisha ya wanafunzi. Kulingana na Nida (2001) ni kwamba, baadhi ya lugha ya mafumbo yanahitaji ufafanuzi unaoafiki lugha pokezi. Isitoshe, lugha ina mizizi inayojikita katika viashiria vya utamaduni wa wenyeji;
- v. Awe mweledi wa lugha lugha zote mbili au zaidi (iwapo kazi husika ni tafsiri ya tafsiri ya lugha nyinginezo) zinazohusika wakati wa kufundisha kuwepo na maelezo angavu ili kuwea kuepukana na vizingiti vya tamaduni zinazohusika.
- vi. Aelewe utaratibu wa ufunzaji wa fasihi-tafsiriwa, kuna haja ya kuzingatia namna na jinsi wakufunzi wanavyofundisha na vitabu vinavyotumiwa;
- vii. Afahamu kimbele, wanafunzi wake walipata mafunzo ya aina gani? Wanapofunzi hudhihirisha utajiri wa fasihi ya kigeni na kudhalilisha fasihi ya Kiswahili ambayo ni ya wenyeji kutokana na yale walivyojifunza katika mazingira ya kigeni. Baadhi ya wahadhiri hao ndio wanaosimamia na wanaoelekeza tasnifu. Wahadhiri hawa ndio wanaowatayarisha na kupanda mbegu za kigeni na matokeo ni kuota na kuendeleza fasihi ya Kiswahili kwa jicho la kigeni. Matokeo ni kuitweza n kuifukarisha fasihi ya Kiswahili na kuikweza fasihi ya kigeni. Kuna haja ya wakufunzi kupata mafunzo zaidi kuhusiana na tafsiri na ufasiri wa tamaduni mbalimbali za kilimwengu. Zaidi ya kufahamu taratibu hizo, somo la fasihi-tafsiriwa litakuwa la kufurahisha na manufaa kwa wanafunzi na matokeo yatakuwa na kuwajenga kitaaluma;
- viii. Kuuelewa ujumbe asilia uliowasilishwa;
- ix. Ujuzi wa lugha zote mbili (asilia na pokezi). Hapa kuna uatata unaoweza kuzka. Baadhi ya tungo huwa zimepitia tafsiri mbalimbali kabla hazijatufikia kwaa Kiswahili;

- x. Kuwa na uwezo wa kufasiri na kurekebisha masuala muhimu yaliyowasilishwa iwapo tafsiri imepotoshwa; na
- xi. Wafahamu malengo ya ufundishaji wa kozi hizi.

Hoja zilizorejelewa hapo juu ni mambo yanayoweza kuzingatiwa katika maandalizi ya awali kwa mkufunzi kabla ya zoezi la kufundisha somo la fasihi-tafsiriwa kwa Kiswahili. Aidha, mkufunzi anahitaji kujiuliza maswali yafuatayo: mtunzi asilia anazungumzia nini? Matarajio ya mtunzi asilia ni kuwasiliana na nani na wapi? Mtunzi asilia analikuwa katika hali gani? Azma ya mtunzi asilia ni nini?. Haya ni baadhi ya maswali ambayo yanamtayarisha mkufunzi kabla ya kukabiliana na wanafunzi wake.

Matatizo katika Ufunzaji wa Fasihi-Tafsiriwa kwa Kiswahili

Ufunzaji wa fasihi-tafsiriwa kwa Kiswahili si kazi nyepesi. Baadhi ya wakufunzi hupitia changamoto kadhaa na hili hupitishwa kwa wanafunzi. Hii ni kwa sababu baadhi ya wakufunzi hawakuandaliwa katika taaluma ya ualimu (BE.D) katika shahada zao bali walisoma Kiswahili na fasihi kwa ujumla yaani (BA). Mpaka sasa, tanzu mbalimbali za fasihi zinaendelea kutafsiriwa kwa Kiswahili. Kutokana na tajriba ya Mukwana (2017) katika tafsiri ya tamthilia ya William Shakespear ya *Othello* ‘Othello: Tanzania ya Mtu Mweusi’, anatahadharisha kuwa, lugha hubadilika kila uchao. Kwa sababu lugha iliyotumika katika matini asilia huweza isieleweke kwa watu wanaoifahamu lugha ya sasa kama inavyobainika katika Kiingereza cha Shakespear. Katika harakati ya kutafsiri, Mukwana ameeleza kuwa ilibidi kuelewa historia, sababu ya kuwasilisha maudhui aliyoshughulikia, muundo wa lugha na mtindo uandishi wa uandishi wa mtunzi asilia. Haya ni baadhi ya mambo ya msingi ambayo mkufunzi anahitaji kuzingatia kabla ya kuviteua na kuvifunza vitabu vya fasihi-tafsiriwa kwa Kiswahili. Swali hapa ni, je wakufunzi hushughulia haya au hutegemea tu maelekezo ya mtafsiri? Kwa sasa fasihi tafsiri kwa Kiswahili zipo na zinafunzwa katika vyuo vikuu. Tafsiri hizo za fasihi kwa Kiswahili zinaweza kuwekwa katika matapo matatu: zile zilizotungwa kwa kuzingatia mazingira asilia ya mataifa ya bara la Afrika na kuwasilishwa kwa lugha ya kigeni kama vile Kiingereza na Kifaransa. Pili, zile zilizotungwa kwa kuzingatia mazingira ya mataifa ya mabara mengine ya ulaya na kuwasilishwa kwa lugha za kigeni za mataifa hayo na kutafsiriwa moja kwa moja kwa Kiswahili. Tatu, zile zilizotungwa kwa kuzingatia mazingira ya ulaya na kutafsiriwa kwa lugha ya kigeni na baadaye kutafsiriwa kwa Kiswahili. Katika kundi la kwanza kuna uwezekano wa kuwepo wa visawe vya kimaana na kitamaduni (mshabaha wa utamaduni unaweza kupatikana kwa lugha pokezi kutokana na tajriba na mazingira sawa ya kimaeneo). Miongoni mwa kazi hizo fasihi ni: *The Devil on the Cross* ‘Shetani Msalabani’ *The River Between*; *Weep Not Child* ‘Usilie Mpenzi Wangu’; *The Beautiful ones are not yet Born* ‘Wema hawajazaliwa’; *Arrow of God* ‘Mshale wa Mungu’; *Betrayal in the City* ‘Usaliti Mjini’ na *Things Fall Apart* ‘Shujaa Okwokwo’. Kundi la pili lina uwezekano wa kupata viwango fulani vya visawe au maelezo kutolewa na mtafsiri

wa Kiswahili. Mifano hapa ni: *Animal Farm*, *Merchant of Venice* na *The Government Inspector*. Kundi la tatu lina changamoto nyingi zinazoweza kumkabili mtafsiri wa Kiswahili. Changamoto katika kundi la tatu zinatokana na sababu kwamba, kuna lugha mbili zilizotumika katika tafsiri kabla ya Kiswahili ambayo ni lugha lengwa na ujumbe na matumizi teule ya lugha yanaweza kukosa kuwiana. Mifano ya kazi hizo za kifasihi ni: *Mkaguzi Mkuu wa Serikali*, *Mabepari wa Venisi*, *Juliasi Kaizari*, *Shamba la Wanyama*, *Antigoni*, *Mfalme Edipode*. Haya ni baadhi ya mambo ambayo yanaweza kuzua utata katika kuufikisha ujumbe kwa Kiswahili (Malangwa, 2005). Matatizo mahsusi yanaweza kuwakabili baadhi ya wakufunzi wa fasihi-tafsiriwa ya kigeni kwa kuzingatia tapo la pili na la tatu ni yafuatayo:

- i. Mkufunzi anahitaji kuzifahamu kazi mbalimbali za fasihi za waandishi asilia na mazingira yaliyowalea na kuwakuza ili kuwa katika nafasi mwafaka katika kufasiri mandhari na hisi zinazowasilishwa kwa ulinganifu na ufaafu wa tungo hizo. Isitoshe, tungo asilia zimejikita lugha zinazobeba tamaduni, itikadi na mielekeo ya waandishi asilia. Vivyo hivyo, tafsiri zenyewe zinaweza kuathiriwa na tamaduni pokezi. Kulingana na Mukwana (keshatajwa), kuna uwezekano wa tafsiri hizo ama kuwa imefaulu au imepotoshwa kutokana na masuala kama vile ya kijamii, kitamaduni, kisiasa, kihistoria, kisera na kimbeko;
- ii. Mkufunzi awe ni mjuzi wa lugha zaidi ya mbili zilizohusishwa katika mchakato wa tafsiri. Kwa kuzingatia hili, mkufunzi atakuwa amejiaandaa katika kuwaelekeza wanafunzi wake kuhusu mawazo asilia katika tafsiri kupitia ya pili au zaidi na mbinu zilizotumika katika Kiswahili, ambayo ni lugha lengwa. Kwa sababu baadhi ya tungo za fasihi asilia huwa zimewasilishwa kwa mizungu ya lugha na tamathali za usemi. Kwa kuingatia haya, itakuwa rahisi kuwaelekeza wanafunzi wasioelewa muktadha wa matumizi ya lugha na ujumbe asilia;
- iii. Mkufunzi atumie vitabu tafsiriwa kwa Kiswahili ambayo vimepitia mchakato wa uhariri na vilivyochapishwa na matbaa zinazotambuliwa na serikali. Aidha, yeye mwenyewe anaweza kuvipitia vitabu hivyo kabla hajaviidhinisha katika ufunzaji wa somo hili. Ikiwa hana ujuzi wa lugha asilia anaweza kutafuta usaidizi kutoka kwa wazungumzaji wa lugha hizo zilizotumika katika tafsiri;
- iv. Wakufunzi wa muda ambao hufunza bila ya tajriba ya fasihi hizo, wasirusiwe kufunza fasihi hizi;
- v. Thamani ya ubora wa kozi fasihi-tafsiriwa hutegemea ujuzi na jitihada za mkufunzi. Sababu ni kwamba, wanafuzi wana matarajio mengi kutoka kwa tungo hizo za fasihi kwa uelekezi wa mkufunzi wao;
- vi. Zaidi ya mkufunzi kuwa na tajriba ya ufunzaji wa fasihi ya Kiswahili anahitaji kuhudhuria makongano na warsha ili kujiendeleza katika taaluma ya tafsiri;

- vii. Wafanye utafiti zaidi badala ya kutegemea yale waliyofunzwa wakiwa wanafunzi wa vyuo vikuu. Sababu ni kwamba, kwa kuzingatia yale waliojifunza, itakuwa ni ukasuku unaoweza kuwafanya wazembe katika kuendeleza kwa usahihi ufunzaji wake wa fasihi-tafsiriwa kwa Kiswahili; na
- viii. Wengine hawajasomea taaluma ya fasihi-linganishi ambayo ni ya msingi katika ufunzaji wa fasihi-tafsiriwa katika ngazi ya vyuo vikuu.

Hayo ni baadhi ya matatizo ambayo yanakumba ufunzaji wa fasihi-tafsiriwa kwa Kiswahili. Hata hivyo, ni mambo amabayo yanaweza kuepukwa kwa kiasi Fulani.

Mustakabali wa Ufundishaji wa Fasihi -Tafsiriwa za Kigeni kwa Fasihi ya Kiswahili Swali hapa ni, ahadi ya fasihi ya kigeni kwa Kiswahili ni nini? Kuna haja ya kuwepo na mabadiliko katika ufunzaji wa fasihi hii. Kwa mfano: wanafunzi wanafunzwa fasihi-tafsiriwa kwa Kiswahili kwa ajili ya mitihani. Zaidi ya hayo, wanafunzi wanahitaji kuelekezwa zaidi katika utafiti wa masuala ibuka na ulinganishaji wa fasihi hizo. Aidha, usomaji usiwe ni wa kujiburudisha tu, bali kujenga mazingira ya shauku ya mfanano wa kimaudhui na masuala ya lugha katika fasihi hizo. Ili wanafunzi wa fasihi-tafsiriwa za kigeni waweze kufurahia na kulienzi somo hili wawe ni:

- i. Wanafunzi wenye ari ya kujifunza fasihi-tafsiriwa ndio wajisajilishe katika somo hilo;
- ii. Wanafunzi wjifunze mbinu za utafiti kuhusu fasihi hii ili kuweza kujiendeleza zaidi katika masuala ya kifasihi; na

Wanafunzi na wahadhiri washiriki katika warsha za mara kwa mara. Warsha hizo ziwe zimeandaliwa na wataalamu wa tafsiri ambo pia ni wahakiki wa fasihi.

Hitimisho

Ulimwengu unazidi kufinyangwa na kuwa kijiji, hivyo basi jitihada za kutafsiri zinahitaji kwenda sambamba na kasi ya utandawazi. Hivyo, ipo haja ya kuhakikisha kuwa tuna kanzi ya istilahi za kutosha za kifasihi, pakiwemo makamusi maalumu yanayolenga kipindi cha historia kilichopo ili kufanikisha tafsiri hizo. Kutokana na teknolojia ya mawasiliano, kazi ya tafsiri huenda ikawa nyepesi. Kinachohitajika ni ushirikiano wa wasomi na wataalamu wa Kiswahili ili kuipigia mbizi shughuli hii.

Isitoshe, mfumko wa istilahi mbalimbali za kifasihi zinazoibuka kila uchao miongoni mwa maandishi na wahakiki wa fasihi ya Kiswahili unahitaji kupitia katika usanifishaji ili kazi ya kutafsiri iwe na uwiano mzuri. Hivi sasa kuna shehena kubwa ya istilahi ghafi ambazo zinatumiwa kiholela tu na wafasiri mbalimbali, na hivyo kuifanya tafsiri ya kifasihi kuwa tata zaidi. Hili linaweza kumtatiza msomaji wa matini za kifasihi zilizotafsiriwa. Watafsiri wa Kiswahili walio na weledi wa lugha za kigeni wanaweza pia kuchukuwa jukumu la kutafsiri kazi za fasihi ya

Kiswahili zilizoko ili ziweze kujulikana nje ya mipaka ya nchi za Afrika Mashariki. Mazao haya ya kifasihi yataenea kwa haraka kutokana na kasi iliyoko ya mawasiliano ya kiteknolojia. Hii itasaidia kusambaza fasihi za nchi zetu kwa mataifa ya ulimwengu. Ipo haja pia ya kutafakari upya nafasi ya fasihi-tafsiriwa kwa Kiswahili katika jumuiya pana ya Afrika ya Mashariki. Kwa mfano, swali ambalo linaweza kuulizwa ni; Je, fasihi hii inaendeleza utamaduni wa kigeni kwa kutumia Kiswahili kutafsiri fasihi za kigeni? Mwisho bali si akali, upo umuhimu wa kuwa na sera madhubuti itakayoelekeza utafsiri ili kudhibiti mfumko wa kazi zinazotafsiriwa kila uchao. Hili litasaidia fasihi tafsiri ya Kiswahili kuweza kuwa na mustakabali mzuri. Hadhira pia inahitaji kuwa angalifu inaposoma baadhi ya kazi zilizotafsiriwa kwani aghalabu hutungwa au kutafsiriwa kwa uelekezi wa hisia za kibinafsi na kiitikadi miongoni mwa watafsiri.

Marejeleo

- Adungo, C. (2018). "Fasihi Haisawiri maisha halisi, ni tokeo la ubunifu wa Mtunzi" katika 'Ukumbi wa Lugha na Fasihi', Gazeti la *Taifa Leo*, Na. 19809. Nairobi: Nation Media Group Ltd. Tarehe 28.3.2018, uk. 10.
- Bakize, L. H. (2013). *Tafsiri na Ukalimani*. Dar es Salaam: Maccony Printers Press.
- Brown, D. H. (2000). *Principles of Language Learning and Teaching*. San Francisco: Pearson Longman.
- Kandagor, M. na Magugu, V. (2017). "Teaching of Translation Studies in Kenyan Universities" katika *Mwanga wa Lugha*. Jarida la Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret: Moi University Press, kur. 53 - 62.
- Maitaria, J.N. na Momanyi, C. (2016). "Dhima ya Fasihi-tafsiriwa ya Kigeni kwa Fasihi ya Kiswahili" katika *Chemchemi Juz.10, Na.2*. Jarida la Chuo Kikuu cha Kenyatta. Nairobi: Kenyatta University Press, kur. 228-244.
- Malangwa, S.P. (2005). "Problems of Translating Lirerary Works: The Case of Julius Kambarage Nyerere's Translation of The Play *Mabepari wa Venisi*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mbaabu, I. (1996). *Language Policy In East Africa*. Nairobi: Educational Research and Publications.
- McAthur, T. (1983). *A Foundation for Language Teachers*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Mohochi, E.S. (2018). "Mchango wa wahadhiri wa muda katika Ufundshaji wa Kiswahili katika vyuo Vikuu nchini Kenya" Makala iliyowasilishwa katika kongamano la Chakama Novemba 23-24, Dodoma. (Haijachapishwa).
- Muigai, M.N. (2005). "Ubunifu wa Mtafsiri: Tamthilia ya Masaibu ya Ndugu Jero." Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

- Mukwana, A. (2017). "Matatizo ya Tafsiri katika kazi za Fasihi: Tajriba Yangu kutokana na tafsiri ya *Othello-Tanzia ya Mtu Mweusi*" katika *Mwanga wa Lugha*. Jarida la Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret: Moi University Press, kur 39-52.
- Mushi, S. (1971). *Mfalme Edipode*. Nairobi. Oxford University Press
- Mutie, E.K. (1997). "Sanaa katika Tafsiri: Matatizo na Athari Zake." Tasnifu ya Uzamili. Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Mwansoko, H.J.M. (1996). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu*, TUKI: Dar es salaam.
- Newmark, P. (1988). *A Textbook of Translation*. London: Prentice Hall.
- Nida, E. A. (2001). *Language and Culture: Context in Translating Shanghai*. Shanghai: Foreign Language Ed Press.
- Njogu, K. & Wafula, R.M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Nyerere, J. K. (1969). *Mabepari wa Venisi*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Odeo, I. (2002). "The Future of Kiswahili Classroom Research" katika Simala (Mhr.) *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press, kur. 128-135.
- Ruhumbika, G. (1985). "Tafsiri za Maandishi ya Kigeni kwa Kiswahili" katika Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili II: Dar es Salaam. TUKI. kur. 83-96.
- Ryanga, C.W (1985). "Vitabu vya Kutafsiriwa na Fasihi ya Kiswahili" katika *KISWAHILI Juz. 52/1&52/2 1985*. Dar es Salaam. kur. 161-174.
- Shitemi, N.L. (1997). "Uaminifu katika Tafsiri: Uhakiki wa Tafsiri za Ushairi wa Jadi wa Kiswahili; Utenzi wa Inkishafi, Utenzi wa Mwanakupona na Mashairi ya Muyaka." Tasnifu ya Uzamifu. Eldoret: Chuo Kikuu cha Moi. (Haijachapishwa).